

MUHULA WA TATU
KIDATO CHA KWANZA 2023
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

UFAHAMU

- a) Ugonjwa wa Covid-19 na makali yake (1×1)
- b) Wanahudumu wa afya walikosa nafasi ya matibabu au nafasi ya kulazwa katika hospitali wanazohudumu wenyewe. (1×1)
- c) - Watu wengi kupoteza kazi zao.
 - Watu wengine kutumwa kwa likizo bila malipo.
 - Wengine kukatwa mishahara kwa asilimia kubwa.
 - Biashara nyingi kufungwa nyingi zikipata hasara chungu nzima.
 - Benki kuathirika kwa wateja kushindwa kulipa mikopo. (3×1)
- d) - Kukohoa
 - Kushindwa kupumua au ugumu wa kupumua.
 - Joto jingi au baridi kali mwilini.
 - Maumivu ya misuli au mwili.
 - Kutapika au kuendsha, kupoteza hisia za kuonja na kunusa. (2×1)
- e) - Kutovaa barakoa kila wakati unapoenda kwenye watu.
 - Kutoosha mikono yako kwa maji yanayotirirka na sabini au kuitakasa.
 - Kwenda kwenye mikusanyiko ya watu.
 - Kutozingatia umbali wa mita moja unapokumbana na watu. (3×1)
- f) - Serikali ilitangaza kufungwa kwa shule.
 - Kafyu ya saa moja usiku hadi saa kumi na moja asubuhi iliwekwa hapo awali.
 - Kufungwa kwa uchukuzi wa kimataifa ilitangazwa.
 - Kudhibitiwa kwa uchukuzi nchini kwa kupunguzwa kwa idadi ya watu kwenye uchukuzi wa uma.
 - Mikusanyiko ya watu ilipigwa marufuku.
 - Kanisa kufungwa japo kwa muda.
 - Idadi ya watu katika arusi na mazishi kupunguzwa mno.
 - Maeneo ya burudani pia yalifungwa kwa muda. (4×1/2)
- g) - Saa za kafyu zilipunguzwa.

- Uchukuzi wa kitaifa na kimataifa ulifunguliwa upya.
 - Shule pia zilianza kufunguliwa japo kwa watahiniwa.
 - Kufunguliwa kwa maeneo ya burudani.
 - Maeneo ya kuabudu yalifunguliwa japo kwa masharti ya kiafya. (2×1/2)
- h) i) Kafyu- Amri ya kutotoka nje nyakati fulani kama vile usiku hadi asubuhi. (1×1)
- ii) Mchakato – Hatua za kufuata wakati wa kufanya jambo (1×1)

SARUFI (alama 40)

1. a) /w/, /y/ (1×1/2)
b) /p/, /b/ (1×1/2)
2. i) ‘ua
ii) kumbu‘kumbu
iii) ‘nafsi
iv) mwana‘funzi (1×1/2)
3. i.walahi- kihisishi (I)
nilimuona kitenzi (T)
Kamau –nomino (N)
nitampiga – kitenzi (T) (4×1/2)
 - ii.mimi – kiwakilishi (W)
nilimwambia –kitenzi (T)
jana – kielezi (E)
asubuhi – kielezi (E) (4×1/2)
4. Mwanzoni mwa sentensi mf. Mwalimu ameingia darasani.
Kuandika nomino za pekee mf. Kenya, Tana, Juma.
(Majina ya watu, milima, mito, miji, nchi, mwezi, siku) (matumizi alama mbili mifano alama mbili)
5. Sanduku LI-YA
Rangi I-I
Uteo U-ZI (3×1)
6. Mwalimu hajakuwa akitufundisha. (2×1)
7. vitate ni maneno yanayotatanisha kimatamshi.

Mfano. Paa baa bata pata (Maana alama moja, mfano alama moja)

8. Kitoto/kijitoto kimevuka kijito kile. (2×1)

9. Mke wake ni mgonjwa.

Nyanya yake ni mgonjwa. (2×1)

10. Ame- viambishi awali

eshwa – viambishi tamati (2×1)

11. Hali timilifu

‘ki’ ya masharti

Wakati uliopo

Wakati ujao (4×1)

12. i) anua

ii) pigana

iii) someshwa

iv) ogofya (4×1)

13. Naf-si

o-a

shu-ku-ru

kwa-o (2×1)

14. Mwalimu mfupi amesimama juu. (2×1)

15. Kiimbo ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti mtu anapozungumza. (1×1)

16. i) Swalii

ii) Mshangao (2×1)

ISIMU JAMII

i) sajili ya hotelini/mkahawani. (Kutaja alama moja sababu alama moja)

ii) matumizi ya msamiati maalum mf. Karanga, sosi

matumizi ya misimu mf. Ukimanga

matumizi ya tanakali za sauti mf. Mate ndo!ndo!ndo!

matumizi ya sentensi fupifupi

lugha ya ucheshi na utani

kuchanganya ndimi

lugha si sanifu. (Kutaja $\frac{1}{2}$ mfano alama $\frac{1}{2}$)

- iii) sajili ya uwanjani
sajili ya darasani
sajili ya kanisani. (2 \times 1)(mwalimi akadilie jibu la mwanafunzi)

FASHI SIMULIZI (ALAMA 15)

1. hadhira- ni wasikilizaji au watazamaji wa kazi yoyote ya fasihi.
Fasihi – ni Sanaa inayotumia lugha kwa ufundi kuwasilisha ujumbe kwa mwanadamu.
Ngano – hivi ni visa vya kubuni au vya kweli ambavyo huwasilishwa kwa lugha kinathari
kuhusu watu, matukio na mahali mbalimbali. (3 \times 1)
2. Fasihi simulizi
Fasihi andishi (2 \times 1)
3. Nyimbo za siasa
Bembea/bembelezi/pembelezi
Nyimbo za kazi/hodiya
Nyimbo za watoto (chekechea)
Nyiso
Nyimbo za sifa (sifa)
Nyimbo za mapenzi. (4 \times 1)
4. Kuhifadhi na kuridhisha maarifa ya jamii.
Husaidia kukuza lugha
Fasihi hupumzisha (huburudisha na huliwaza)
Fasihi ni kitambulisho cha jamii za binadamu
Husaidia kukuza au kujonga tabia
Kumburudisha na kumstarehesha binadamu
Kuichochua na kuelimisha jamii
Huadilisha/kukuza maadili
Huunganisha na kuibua hisia za mzalendo. (6 \times 1)